

Sera ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha

Sera hii inatumika kwa shughuli zote za kimatibabu za Huduma za Afya ya Kiakili za Kikistro za Pine Rest (Pine Rest) na watoa huduma wote wanaotumiwa na Pine Rest.

Tarehe ya Kuanza Kutumika: Mei 1, 2018

Ilani ya Kutobagua: Pine Rest inaambatana na sheria husika za serikali kuu za haki za umma na haibagui kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu, au jinsia. Pine Rest haitengi watu wala kuwachukulia kwa njia tofauti kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu au jinsia. Tazama [Ambatisho A](#) ili kupata ilani kamili ya kutobagua na vile vile upatikanaji wa usaidizi wa lugha.

I. Madhumuni

Madhumuni ya sera hii ni kubainisha mchakato unaofuatwa ili kubainisha ni nani anastahiki kupokea usaidizi wa kifedha katika Pine Rest; kuelezea upatikanaji wa usaidizi wa kifedha kwa wagonjwa na kwa umaa; na kuhakikisha kwamba miongozo husika inatumika kwenye maombi ya usaidizi wa kifedha, bila kujali eneo la Pine Rest ambako huduma ya mgonjwa inatolewa.

II. Majukumu

Sera ya hii ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha itawasilishwa na mhudumu mteule wa Pine Rest kama ilivyobainishwa katika taratibu ambatanishi.

III. Filosofia

Filosofia ya Pine Rest ni kutoa huduma zenye ubora za afya ya kitabia kwa wote wanaokuja kwetu wakitaka usaidizi. Mahitaji ya matibabu yatabainishwa na mtoa huduma anayetibu. Maamuzi ya usaidizi wa kifedha yatatolewa kulingana na hitaji la kifedha linaloonyeshwa na usaidizi utaidhinishwa kwa ushirikiano na mgonjwa/dhamini. Wagonjwa/wadhamini wote wanaotuma maombi ya kifedha watapitia mchakato sawia wa usaidizi wa kifedha bila kujali mlipaji msingi.

IV. Sera ya Huduma ya Matibabu ya Dharura

Pine Rest, bila ubaguzi, itatoa huduma kwa hali za matibabu ya dharura kwa watu bila kujali uwezo wao wa kulipa au ustahiki wa kupokea usaidizi wa kifedha. Pine Rest haitajihusisha katika hatua zinazowafanya watu kutotafuta huduma za matibabu ya dharura, na, ili kufanikisha hili, huduma ya dharura itatolewa bila kudakizwa na shughuli ya ulipishaji deni au madai ya malipo kwa huduma kabla ya matibabu kutolewa.

V. Sera

A. Maelezo Jumla

1. Kabla ya kutafuta usaidizi wa kifedha, mgonjwa/mdhamini pamoja na Pine Rest watapitia mbinu zote za malipo zinazotolewa na wahusika wengine.
2. Ni sera ya Pine Rest kudai malipo kamili kwa huduma zote zinazotolewa.
3. Wagonjwa/wadhamini wanaotambua kwamba hawajiwezi kifedha, au wametambuliwa na Pine Rest kuwa hawajiwezi kifedha, watatumwa kwa wahudumu mwafaka ili ukaguzi ufanywe, kama inavyohitajika. Mhudumu wa Pine Rest huenda akaendelea na mchakato wa kufanya ombi la usaidizi wa kifedha ili kubaini ukosefu wa uwezo wa kulipa. Mgonjwa/mdhamini huenda akaombwa ajaze ombi la usaidizi wa kifedha. Ripoti ya

ulipaji madeni huenda itapitiwa ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa kwenye ombi, lakini haitatumiwa kufanya uamuzi wa ustahiki wa kupokea usaidizi wa kifedha. Sehemu kadhaa za mchakato wa ombi la kifedha au mchakato mzima huenda ukatupiliwa mbali kwa wagonjwa/wadhamini fulani ambao tayari wanahitimu kupokea usaidizi wa kifedha na wameshaa thibitishwa, na kama inavyoambatana na sera na taratibu za Pine Rest. Mifano huenda ikajumuisha watu wanaochukuliwa kuwa bila makazi au waliofariki bila mali yoyote.

4. Kama tokeo la mchakato wa ombi la kifedha, ikiwa vigezo vya usaidizi havijafikiwa, mgonjwa/mdhamini atashauriwa kupanga malipo kulingana na [Sera ya Bili za Wagonjwa na Ulipishaji Deni](#) ya Pine Rest na taratibu husika kwa ambazo mgonjwa/mdhamini huenda akahitimu kupata mapunguzo na/au mbinu nyingine za malipo kama vile mapunguzo ya malipo ya haraka au mipango ya malipo.
5. Ikitokea kwamba miongozo ya matatizo ya kifedha huenda ikatumiwa, mgonjwa/mdhamini huenda akaombwa atoe rekodi ambatanishi na ombi litasindikwa ipasavyo.
6. Matokeo ya uamuzi yatarekodiwa kwenye akaunti ya mgonjwa. Juhudi mwafaka zitafanywa ili kumfahamisha mgonjwa/mdhamini kwa maandishi kuhusu maamuzi (ikijumuisha, ikiwa inahitajika, usaidizi ambao anastahiki kupokea) na msingi wa maamuzi.
7. Rekodi zote husika na ambatanishi za maombi zitahifadhiwa kulingana na sera za kuhifadhi hati.

B. Vyanzo vya Malipo ya Wahusika Wengine

Kabla ya kutafuta usaidizi wa kifedha, mgonjwa/mdhamini pamoja na Pine Rest watapitia mbinu zote za malipo zinazotolewa na wahusika wengine ikijumuisha lakini sio tu Medicaid and usajili katika Health Insurance Exchanges (Soko la Bima za Afya). Pine Rest inahifadhi haki ya kuchunguza, kudhibitisha kufanya mahojiano na kuomba kutolewa kwa:

1. Manufaa yote kutoka kwa chanzo chochote cha bima nyingine;
2. Manufaa yote kutoka kwa miradi ya usaidizi wa serikali kuu ambayo kwa mgonjwa/mdhamini ana ustahiki wa kupata;
3. Manufaa yote kutoka kwa shirika lolote la misaada; na/au
4. Kesi zote zilizosubirishwa.

Usaidizi wa kifedha ndio suluhu ya mwisho kabisa ya akaunti. Hivyo basi, mgonjwa/mdhamini ni lazima atimize majukumu yote chini ya miradi yoyote husika iliyotajwa hapa juu au atumie rasilimali zilizopo kabla ya kuhitimu kupata usaidizi wa kifedha. Mgonjwa/mdhamini kukosa kutoa maelezo hitajika au kushiriki katika mojawapo ya miradi iliyo hapa juu huenda kukapelekea kunyimwa usaidizi wa kifedha.

C. Upatikanaji wa Usaidizi wa Kifedha

Pine Rest imeweka mikakati ya kuwasiliana na wagonjwa na umma kuhusu upatikanaji wa usaidizi wa kifedha. Mbinu za mawasiliano zinajumuisha lakini sio tu maelezo katika ofisi ya/za mapokezi, vyumba vya kusubiri na maeneo mengine ya umma, na pia maelezo yaliyo kwenye tovuti ya Pine Rest. Aidha, Pine Rest itatoa muhtasari rahisi wa Sera yake ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha kama sehemu ya mchakato wa kuwapokea na/au kuwaruhusu wagonjwa kuondoka, na pia kuwapa watu usaidizi katika kukamilisha

mchakato wa kutuma ombi.

Wagonjwa wataarifiwa kuhusu Sera ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha kwenye ripoti zao za bili kwa kipindi cha angalau siku 120 tangu siku ya kwanza ya ripoti ya bili ya baada ya kuondoka. Madeni ya wagonjwa yatastahiki kufanyaiwa ukaguzi wa usaidizi wa kifedha kwa kipindi cha angalau siku 240 tangu siku ya kwanza ya ripoti ya bili ya baada ya kuondoka ("Kipindi cha Ombi"). Pine Rest ikipokea ombi la usaidizi wa kifedha wakati wa Kipindi cha Ombi, iwe ombi hilo ni kamili au la, itaahirisha shughuli zote za ulipishaji deni mpaka wakati maamuzi kuhusu usaidizi wa kifedha yatafanywa.

D. Mchakato wa Kutambua Usaidizi wa Kifedha nana Kutuma Ombi

Lengo la mchakato wa ustahiki wa kupokea usaidizi wa kifedha ni kubainisha uwezo wa mgonjwa/mdhamini wa kulipa. Nakali ya bila malipo ya Sera ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha, na pia [ombi la usaidizi wa kifedha](#) la sasa na [muhtasari wa sera kwa lugha rahisi](#), zinapatikana kwenye vituo vya kimatibabu vya Pine Rest, kwenye <https://pinerest.org/about-us/financial-assistance>, kwa kupiga simu kwa nambari (616) 455-5019 au kutuma barua pepe kwa mshauri wa kifedha kwa anwani patientaccounts@pinerest.org. Kila mtu huenda akahitajika kujaza ombi la usaidizi wa kifedha na kutoa maelezo ambayo Pine Rest imeagiza kama sehemu ya ombi. Pine Rest inabainisha usaidizi wa kifedha kulingana na miongozo ya matatizo ya kifedha yaliyobainishwa katika sera hii.

E. Rekodi Ambatanishi za Kifedha

Huenda Pine Rest inahitaji nakala za stakabadhi za malipo, rekodi za ulipaji ushuru na vyanzo vingine vyoyote vya kuthibitisha mapato na mali. Teknolojia huenda ikatumiwa ili kusaidia kuwatambua wagonjwa wanaohitimu kupokea usaidizi kwa njia amilifu na fanisi au ili kurahisisha mchakato wa kupata data na uchambuzi unaohitajika wa uwezo wa kulipa. Watuma maombi huenda wakaombwa wasaidie na washirikiane katika kutuma ombi la manufaa kutoka kwa bima nyingine husika, miradi ya misaada ya jimbo, serikali kuu au mingine iliyotajwa hapo awali.

F. Vigezo vya Uhitimu vya Miongozo ya Matatizo ya Kifedha

Katika kubainisha ustahiki wa kupokea usaidizi wa kifedha, Pine Rest itakagua uwezo wa mgonjwa/mdhamini wa kufidia Pine Rest kwa huduma zinazoagizwa au zilizotolewa hapo awali.

Pine Rest itakagua maelezo kama yafuatayo:

1. Viwango vya mapato
2. Thamani ya utajiri
3. Hadhi ya ajira
4. Majukumu mengine ya kifedha
5. Kiwango na marudio ya bili za huduma ya afya

Ripoti ya ulipaji madeni huenda ikapitiwa ili kuthibitisha maelezo. Pine Rest itatumia Miongozo ya sasa ya Umaskini ya Serikali Kuu ya Marekani kama msingi wa vigezo vya uhitimu vya ustahiki wa kimapato. Punguzo la hadi 100% litatolewa kulingana na pato la kaya kwa wale ambao wana pato lisilozidi 250% ya Miongozo ya mwaka huo ya Umaskini ya Serikali Kuu. Rekodi za kifedha zinazohusu pato la kaya ya mgonjwa/mdhamini pia

huenda zikaagizwa, sio ili kumpa mhusika mwingine kazi, lakini ni ili kubainisha jinsi zinavyoathiri hali ya kifedha ya mtuma ombi moja kwa moja. Kaya, kama inavyobainishwa na Ofisi ya Sensa ya Marekani, ni kundi la jamaa wawili au zaidi wa familia moja, wanaohusiana kwa kuzaliwa, ndoa, utwaaji, au vinginevyo, ambao wanaishi pamoja (watu ambao si jamaa wa familia moja, kama vile wanaoshiriki nyumba, hawajumuishwi hapa); watu wote ambao wana uhusiano wanaoishi katika kaya moja wanachukuliwa kuwa jamaa wa kaya moja. Pine Rest haiwachukulii watu ambao wanaishi katika nyumba moja lakini kila mtu ako kivyake na anajikimu kivyake kuwa ni kaya moja. Hali ya kuishi isiyo ya kudumu kutokana na hali ya kimatibabu pia haitazingatiwa. Historia ya kimatibabu, kitabia na/au kijamii ya mgonjwa haitazingatiwa katika kutathmini uwezo wa kulipa.

G. Usawa

Ili kuhakikisha matumizi sawia ya sera hii ndani ya Pine Rest, yafuatayo yanatumika katika vituo vyote husika vya Pine Rest:

1. Ada zote zitarekodiwa kwenye akaunti ya mgonjwa kulingana na taratibu za kawaida za kutoza ada. Ingawa ada ndizo msingi wa uwekaji rekodi za bili na ulipishaji madeni, gharama (si ada) na pia orodha ya ada za Medicare ikiwa zinapatikana, zitakuwa kitengo msingi cha ripoti katika kutathmini thamani ya usaidizi wa kifedha.
2. Ada za huduma “hazitapunguzwa”.
3. “Heshima ya kitaalamu” haitatumika.
4. Pine Rest haitabagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya utaifa, jinsia, dini, umri, ulemavu, imani za kisiasa, mwelekeo wa kimapenzi, na hadhi ya ndoa au familia.
5. Wagonjwa wanatimiza vigezo vya sera hii na wale ambao wameidhinishwa kupokea usaidizi wa kifedha watastahiki kupata huduma za dharura bila malipo au huduma zinazohitajika kimatibabu bila malipo wakati wa kipindi cha idhini kilichobainishwa katika Sehemu ya 6.9. Kwa sababu Pine Rest haitozi ada yoyote kwa wagonjwa wanaostahiki kupata usaidizi wa kifedha chini ya sera hii, Pine Rest inaambatana kikamilifu na “viwango vilivyo kwenye bili” na vipimo vya ada za chini zinazotumika kwa hospitali za misaada.

H. Mchakato wa Kuidhinisha Ombi

1. Maamuzi yote ya usaidizi wa kifedha ni lazima yaidhinishwe na mhudumu mwafaka kama ilivyobainishwa katika Taratibu za Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha.
2. Rekodi ambatanaishi zinapaswa kuandamana na marekebisho yote ya usaidizi wa kifedha.

I. Kipindi cha Idhini

Uidhinishaji wowote wa maombi yote ya usaidizi wa kifedha ni lazima uliofanywa chini ya Sera ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha unaweza kuwa halali kwa kipindi cha angalau siku 90 na unajumuisha huduma zinazofuata za dharura au zinazohitajika kimatibabu. Badiliko katika hali ya kifedha au ongezeko la ustahiki wa mlipaji mwingine huenda likaathiri kipindi cha idhini na kuhitaji mapitio zaidi.

J. Mchakato wa Kukata Rufaa

Watu wanaonyimwa usaidizi wa kifedha chini ya misimamo ya sera hii wanaweza kuomba maamuzi yarudiwe tena. Marudio yatafanywa katika ngazi inayofuata ya mamlaka ya idhini.

Rufaa zinazotumwa juu ya ngazi ya menejimenti ndani ya Akaunti za Mgonjwa zinapelekwa kwa jopo la uongozi mkuu wa Pine Rest lililochaguliwa na Afisa Mkuu wa Kifedha wa Pine Rest au mwakilishi wake mteule.

K. Juhudi za Ulipishaji Deni katika Tukio la Kutolipa

Endapo Mgonjwa/mdhamini hatumi ombi au hahitimu kupokea usaidizi wa kifedha chini ya sera hii, hatua za ulipishaji deni ambazo Pine Rest inaweza inatumia kwa ajili ya malipo kukosa kufanywa zimeelezewa kwa kina zaidi katika [Sera ya Bili za Wagonjwa na Ulipishaji Deni](#). Nakala ya bila malipo ya sera hii inaeza kupatikana kwenye vituo vya Pine Rest, kwenye <https://pinerest.org/about-us/financial-assistance> kwa kupiga simu kwa nambari (616) 455.5019 au kutuma barua pepe kwa anwani patientaccounts@pinerest.org. Ilani tofauti kwa maandishi itatolewa kwa kila mtu kwa angalau siku 30 kabla ya hatua zozote za ulipishaji deni kuanzishwa.

L. Msingi wa Kuhesabu Viwango vya Bili

Pine Rest inatumia mbinu ya kutazama historia kulingana na madai yanayoruhusiwa na huduma ya Medicare ya ada-kwa-huduma katika kipindi cha awali cha miezi kumi na miwili ili kubainisha Viwango vya Bili (Amounts Generally Billed, AGB).

Pine Rest haitozi bili au haitarajii malipo ya ada jumla kutoka kwa watu wanaohitimu kupokea usaidizi wa kifedha chini ya Sera hii ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha.

VI. Marekebisho

Pine Rest inahifadhi haki ya kubadilisha, kurekebisha, au kuondoa sera hii wakati wowote bila ilani ya awali kwa maandishi. Marekebisho yote kwenye viambatisho vyovyote vya sera hii ni wajibu wa Mkurugenzi wa Akaunti za Wagonjwa.

VII. Utengenezaji Sera na Uidhinishaji:

Mmiliki Hati:

Paul H. Karsten, Afisa Mkuu wa Kifedha

Msimamiaji Hati:

Andrea Schachow, Mkurugenzi wa Akaunti za Wagonjwa

Muidhinishaji:

Mark Eastburg, Afisa Mkuu Mtendaji

Ambatisho A

Ilani ya Kutobagua:

Pine Rest inaambatana na sheria husika za Serikali Kuu za haki za umma na haibagui kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu, au jinsia. Pine Rest haitengi watu wala kuwachukulia kwa njia tofauti kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu au jinsia.

Pine Rest:

- Inatoa misaada na huduma za bila malipo kwa watu walio na ulemavu ili wawasiliane nasi kwa ufanisi, kama vile:
 - Wakalimani waliohitimu wa lugha ya ishara
 - Maelezo kwa maandishi katika mifumo mingine (chapa kubwa, sauti, mifumo inayofikika ya kielektroniki, mifumo mingine)
- Inatoa huduma za lugha bila malipo kwa watu ambao lugha yao msingi si Kiingereza, kama vile:
 - Wakalimani waliohitimu
 - Maelezo yaliyoandikwa kwa lugha nyingine

Ikiwa unaamini kwamba Pine Rest imeshindwa kutoa huduma hizi au imebagua kwa njia nyingine kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu, au jinsia, unaweza kuandikisha lalamishi na:

Director, Patient Accounts
517 36th Street
Grand Rapids, MI 49503
616-455-5019; simu bila malipo: 1-800-422-4215
patientaccounts@pinerest.org

Unaweza kuandikisha lalamishi wewe mwenyewe au kwa barua, faksi, au kwa barua pepe. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuandikisha lalamishi, Mkurugenzi wa Akaunti za Wagonjwa yupo akusaidie.

Pia unaweza kuandikisha lalamishi la haki za umma na Idara ya Huduma ya Afya na Wanadamu ya Marekani, Ofisi ya Haki za Umma, kwa njia ya kielektroniki kupitia Lango la Malalamishi la Ofisi ya Haki za Umma, linalopatikana kwenye <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/portal/lobby.jsf>, au kwa kutuma barua au kupiga simu kwa:

U.S. Department of Health and Human Services
200 Independence Avenue SW, Room 509F, HHH Building
Washington, DC 20201
1-800-368-1019, 800-537-7697 (TDD).

Fomu za malalamishi zinapatikana kwenye <http://www.hhs.gov/ocr/office/file/index.html>.